



CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR (SUZA)

TANGAZO KWA WAOMBAJI WALIOCHAGULIWA KUJIUNGA NA SUZA KATIKA MWAKA WA MASOMO 2023/2024

UTANGULIZI

Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kinapenda kuutaarifu umma kuwa kimetoa orodha ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na masomo katika ngazi ya Astashahada (**Certificate**), Stashahada (**Diploma**) na Shahada ya kwanza (**Degree**) kwa mwaka wa masomo 2023/2024 kwa program mbalimbali.

BARUA YA UDAHILI NA VIAMBATANISHO VYENGINE

SUZA inawaomba waombaji wote waliochaguliwa wahakikishe wanaingia katika akaunti zao walizotumia wakati wa kufanya maombi ya chuo (baruapepe/*email na password iliyotumika wakati wa kuomba*) kwa lengo la kupata barua za udahili (**Admission letter**) pamoja na viambatanisho vyengine muhimu vya kujiunga na chuo.

WALIODAHILIWA CHUO ZAIDI YA KIMOJA (MULTIPLE SELECTION)

Kwa waombaji wa shahada ya kwanza (**Degree**) ambao wamechaguliwa chuo zaidi ya kimoja (**multiple selection**), wanashauriwa kuingia katika akaunti zao na kuthibitisha (**confirmation**) kwa kutumia nambari ya siri (**confirmation code**) ambayo wamerushiwa na Tume ya Vyuho Vikuu Tanzania (TCU) kupitia nambari zao za simu au barua pepe walizotumia wakati wakiomba chuo. Kama bado hujatumiwa nambari ya siri, ingia kwenye akaunti na uiombe kupitia sehemu iliyoandikwa **request**

confirmation code. Unatakiwa kufanya uthibitisho mara tu baada ya kupokea (**confirmation code**).

KUFUNGULIWA KWA DIRISHA LA TATU LA MAOMBI

Chuo kinawataarifu wale wote waliochaguliwa katika dirisha la kwanza, pili na tatu kuanza kufanya vipimo vya afya (**Medical Checkup**) na kuripoti chuoni siku ya Jumatatu ya tarehe **23/10/2023** saa tatu (3:00) kamili za asubuhi kwa ajili ya "**Orientation**".

HITIMISHO

SUZA inawaomba wale wote waliochaguliwa wasisite kuwasiliana na maafisa udahili kwa maelekezo/msaada zaidi.

KARIBUNI SUZA

Tangazo hili limetolewa na:

Kurugenzi ya Shahada za Awali (DUS)

Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA)